# Changamoto za Kuingiza Antonimu katika Kamusi Wahidiya za Kiswahili: Mifano kutoka Kamusi Kuu ya Kiswahili Toleo la Tatu (KKK3)

*Jeremiah Swallo Andrew na Musa M. Hans*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Makala haya yamechunguza changamoto za kuingiza antonimu katika fasili za vidahizo vya kamusi wahidiya za Kiswahili. Data zilikusanywa maktabani kwa njia ya usomaji matini. Matini iliyosomwa kwa ajili ya mifano ni Kamusi Kuu ya Kiswahili Toleo la Tatu (KKK3). Vidahizo 379 kati ya 22675 vya KKK3 vilibainika kuwa vimetumia antonimu kufafanua maana zake. Vidahizo vilivyokusanywa vilitumika kama data kushadidia hoja. Data hizo zimechanganuliwa kwa kutumia mikabala ya kitaamuli na kitakwimu. Aidha, Nadharia Jumuishi ya Leksikografia aliyoiasisi Herbert Wiegand imeongoza uchanganuzi wa data. Nadharia hii imeegemea kwenye misingi inayohusu kujali mahitaji ya walengwa wa kamusi, matumizi ya maarifa ya nadharia nyingine nje ya leksikografia na kuangalia kamusi kwa kuzingatia kanuni asilia za wanaleksikografia tangulizi. Makala yamebainisha changamoto za antonimu kileksikografia. Mosi, ni kubadilika kwa kategoria ya kidahizo na antonimu. Pili, ni ukosefu wa urari wa idadi ya antonimu ndani ya kitomeo. Tatu, ni ukosefu wa urari wa mpangilio wa antonimu ndani ya vitomeo. Nne, ni kutozingatia alama za uakifishi. Tano, ni kuwapo kwa upendeleo wa kileksikografia. Sita, ni mpishano wa kidhana kati ya kidahizo na ufafanuzi wake unaohusu antonimu. Makala yanapendekeza watungaji wa kamusi wazingatie kanuni za kufafanua vidahizo vya kiantonimu kwa namna isiyomsumbua mlengwa wa KKK3 kuzing'amua maana zilizokusudiwa kumfikia.**

**Maneno Muhimu**: *Antonimu, Nadharia Jumuishi ya Leksikografia, Vidahizo, Kamusi Wahidiya*,

## Utangulizi

Maana za vidahizo huelezwa kwa kutumia njia mbalimbali ili kuifanya kamusi iliyotungwa ieleweke kwa watumiaji waliolengwa. Miongoni mwa njia za uelezaji wa maana hizo ni matumizi ya antonimu, ambazo kimsingi huhusisha matumizi ya vinyume vinavyohusiana na kidahizo kinachofafanuliwa. Wataalamu kama vile Paradis & Willners (2011) na Bezuglova (2020) wanasisitiza kuongeza umakini wakati wa kuziingiza antonimu ndani ya kamusi ili kunogesha umbo la kamusi husika pamoja na kujenga maana isiyomtatiza mlengwa wa kamusi hiyo. Maana hizo za unyume huegemezwa kwenye mambo yanayohusu idadi ya antonimu ndani ya kitomeo, mpangilio wake, muundo ama umbo lake, matumizi ya viakifishi vinavyohusu antonimu hizo, urejeleano wa kimaana na uhusiano wa kikategoria kati ya kidahizo na antonimu husika. Kuwapo kwa vipengele hivyo miongoni mwa taarifa nyingine za kileksikografia husababisha changamoto za kiutendaji kwa baadhi ya watungaji wa kamusi wahidiya ikiwa ni pamoja na *Kamusi Kuu ya Kiswahili Toleo la Tatu (KKK3)* iliyotungwa na BAKITA mwaka 2022.

## Muhtasari wa Mapitio ya Maandiko kuhusu Uingizaji wa Antonimu katika Kamusi

Antonimu ni neno lenye maana inayokinzana na jingine kiunyume (Jones, 2002; Okal, 2019; TUKI, 2019). Neno antonimu lilibuniwa miaka ya 1860 na Smith alipoandika '*A Complete Collection of Synonyms and Antonyms*' (Jones, 1986; Okal, 2019). Matumizi ya antonimu yalijitokeza karne ya 19 kwenye kamusi za Kijerumani na Kifaransa zilizoandikwa na Paul Ackerman alipokuwa akijaribu kuonesha uhusiano hasi wa maneno unavyoweza kuimarisha maana za maneno mbalimbali (Sterkenburg, 2003). Kuwapo kwa antonimu ndani ya fasili kulisababisha wanaleksikografia waone haja ya kuweka taratibu za jinsi ya kushughulikia uhusiano huu wa kifahiwa katika vitomeo vya kamusi (hasa wahidiya) kwa kupendekeza kanuni mbalimbali zilizoegemea kutafuta umajumui wa kileksikografia. Wataalamu kama vile Lehrer (1974) wanapendekeza antonimu zote zilizotumika

katika kamusi ziorodheshwe na kuonekana kama kijenzi kimojawapo cha sherehe ya kamusi iliyotungwa.

Wataalamu wengine kama vile Fellbaum (1995) wanapendekeza antonimu ziingizwe mwishoni mwa aya za kileksikografia mara baada ya taarifa na ufafanuzi unaohusu kidahizo husika. Maelezo yake ni sawa na Keifer & Sterkenburg (2003) kwamba, antonimu hupaswa kuonekana ama kuingizwa kama viziada vya kitomeo vya kamusi husika. Hata hivyo, mapendekezo yao yanapingwa na Bowern (2008) anaposema, antonimu ni kijenzi cha lazima kujitokeza katika fasili ya neno lolote lenye asili ya kubeba unyume ndani yake.

Naye, Jackson (2002) anaeleza kuwa antonimu hufaa zaidi kueleza maana za vidahizo vya kategoria ya kivumishi ukilinganisha na kategoria nyinginezo kama vile nomino na vitenzi. Anasema miundo ya vivumishi huhitaji antonimu katika fasili zake kwa kuwa uelezaji wake hujikita kwenye ulinganifu wa taarifa zinazopatikana katika kidahizo (kifasiliwa) na antonimu (kifasili). Katika muktadha huu wa kisemantiki watungaji wa kamusi hujikuta wamevifasili vidahizo vya kategoria hii kwa kuegemea zaidi kwenye matumizi ya antonimu.

Pia, suala la idadi ya antonimu ndani ya kitomeo hupaswa kuwa ni msingi muhimu wa kushughulikia fahiwa za unyume katika kamusi (Lobanova, Tom & Jennifer, 2010). Watungaji wa kamusi wanatakiwa kuwa na mwongozo utakaorahisisha maamuzi yao juu ya kiasi cha taarifa za kiantonimu zinazopaswa kuingizwa katika kamusi kutegemeana na vidahizo husika. Antonimu zinazoingizwa huweza kutofautiana kiidadi baina ya vidahizo. Vipo vyenye antonimu moja tu, vingine vina zaidi ya moja. Kwa kuwa yapo mazingira ya baadhi ya vidahizo kuwa na antonimu zaidi ya moja, watungaji wa kamusi hupaswa kuwa na mwongozo wa kuamua muafaka wa idadi ya wastani ya antonimu inayotakiwa kutumika katika toleo husika la kamusi. Kuweka mipaka ya kiidadi husaidia kuamua taarifa zipi haswa ziingizwe kwenye kila kidahizo na kupunguza uholela.

Vilevile, Paradis & Willners (2011) wanasema antonimu zinazoingizwa katika kamusi hazipaswi kupishana sana kiumbo (saizi) na kidahizo husika. Wanachosisitiza ni kutotumia maneno marefu au mengi zaidi ya kidahizo. Inapotokea kidahizo ni neno huru hata antonimu yake inapaswa kuwa neno huru na siyo mwambatano wa maneno zaidi ya lile lililoibua dhana inayohitajika. Mapendekezo yao hayawezi kutumika katika vidahizo vyote kwa sababu lugha hutofautiana kimuundo hivyo mofolojia ya antonimu ama vidahizo huweza kutofautiana kutegemea asili ya maneno husika na dhana zilizofumbatwa kwenye maneno hayo.

Aidha, Fellbaum (2016) amechunguza ushughulikiaji wa maneno katika kamusi na kupendekeza kuingiza antonimu kwa kutumia leksimu za jumla zinazoonesha unyume ulioambatanishwa katika ufafanuzi. Kinachopendekezwa hapa ni matumizi ya ukanushi wa kileksika ambapo antonimu hudokezwa kwa kutanguliwa na vikanushi. Kwa mfano; **zuri** ni isiyokuwa *mbaya*; isiyo*chukiza*. Katika mfano huo, maneno yaliyopigiwa mstari kwa chapa ya italiki yanadokeza antonimu. Maoni haya ni marekebisho ya Fellbaum (1995) baada ya kufanya mapitio zaidi na kupata maoni ya wanaleksikografia wengine. Licha ya kupendekezwa matumizi ya vikanushi, baadhi ya wanaisimu huona si kanuni inayofaa kuitambulisha antonimu katika kamusi kwa sababu mtumiaji wa kamusi huweza kuibeba tu kanuni hiyo na kutambulisha ukanushi badala ya antonimu.

Kadhalika, wataalamu kama vile Okal (2019) wanapendekeza kuwapo kwa urari wa kikategoria kati ya kidahizo na antonimu zilizotumika kukifasili. Mabadiliko ya kikategoria huweza kuathiri uzito wa maana inayobebwa na leksimu husika ingawa undani ama kiini cha maana huweza kubakia vilevile. Mlengwa wa kamusi hutegemea kuipata maana ya kidahizo kwa kuzingatia maneno yaliyotumika kuiunda fasili husika. Katika muktadha wa makala haya, antonimu zilizotumika kukifasili kidahizo hazipaswi kubadilika kikategoria ili kubeba uzito uleule wa kimaana uliokusudiwa kufikishwa kwa mlengwa wa kamusi husika.

Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa baadhi ya watungaji wa kamusi hujikuta wamezikiuka kanuni hizo majumui kiasi cha kuweza kumtatiza mlengwa wa kamusi kuipata maana hasa ya kidahizo kwa namna ya unyume. Kuzikiuka kanuni msingi za kutomesha vidahizo vyenye asili ya unyume kumesababisha kuwapo kwa changamoto mbalimbali ambazo ndiyo kiini cha mjadala wa makala haya.

**Mbinu za Ukusanyaji Data**

Data za makala haya zimekusanywa maktabani kwa njia ya usomaji wa matini. Matini iliyosomwa na kuhakikiwa ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili Toleo la Tatu* (KKK3) iliyotungwa na BAKITA mwaka 2022. Matini hii ilisomwa kwa kuangazia zaidi taarifa zinazohusu antonimu (unyume). Data zilizokusanywa zilitokana na kidokezo cha mwongozo wa mtumiaji wa KKK3 kuhusu antonimu pamoja na maarifa mahususi aliyonayo mtafiti katika kuvipambanua vidahizo vyenye asili ya unyume. Jumla ya vidahizo 379 vimepatikana vikiwa vimefasiliwa kwa kutumia vinyume mbalimbali kuanzia herufi 'A' hadi 'Z' ingawa herufi 'Y' haina kidahizo hata kimoja chenye fasili ya unyume. Jumla ya vidahizo 23 vimeoneshwa katika jedwali Na. 1 ili kuviwakilisha vingine vilivyotumia antonimu kufasili maana zake. Uwakilishi huo umezingatia uteuzi wa kidahizo cha kwanza chenye antonimu kilichojitokeza kwenye herufi 23 zinazohusika.

**Jedwali Na. 1: Mfano wa Vidahizo vya KKK3 Vyenye Antonimu**

| Na | Kidahizo | Antonimu Zilizotumika katika Ufafanuzi wa Kidahizo husika | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Antonimu 1 | Antonimu 2 | Antonimu 3 | Antonimu 4 | Antonim 5 |
| 1 | Aali | Duni | - | - | - | - |
| 2 | Baathi[1] | Fisha | - | - | - | - |
| 3 | Chache | Wingi | - | - | - | - |
| 4 | Dada | Kaka | - | - | - | - |
| 5 | Embamba | Nene | Nzito | - | - | - |
| 6 | Fidhuli | Adabu | Heshima | Nidhamu | - | - |
| 7 | Gatua | Gatisha | - | - | - | - |
| 8 | Hafidhina | Mwanausasa | Mmamboleo | Mwanamageuzi | Mpenda mabadiliko | - |
| 9 | Imara | Dhaifu | - | - | - | - |
| 10 | Jahili[1] | A-huruma | - | - | - | - |
| 11 | Kabwela | Wa-kipato | - | - | - | - |
| 12 | Lila | Fila | - | - | - | - |
| 13 | Madhila | Raha | Furaha | Ureda | Utamu | Burudani |
| 14 | Naam! | Abee! | Bee! | Beka! | - | - |
| 15 | Ovyo | A-utaratibu | - | - | - | - |
| 16 | Pakia | Pakua | - | - | - | - |
| 17 | Rahisi | Ghali | Ugumu | Imara | - | - |
| 18 | Sahau | Kumbuka | - | - | - | - |
| 19 | Taratibu | Haraka | - | - | - | - |
| 20 | Uakuaji | Uachiaji | - | - | - | - |
| 21 | Vita | Amani | Utulivu | - | - | - |
| 22 | Wadhiha | Enye-kificho | - | - | - | - |
| 23 | Zikua | Zika | - | - | - | - |

**Chanzo**: BAKITA (2022)

Antonimu hizi zimetokana na vidahizo vya KKK3 ambavyo mpangilio wake umezingatia muundo wa vidahizo vyote kialfabeti. Data zilizokusanywa zimetumika kushadidia hoja mbalimbali zinazohusu makala haya. Matumizi ya data hizi yamefanyika kinasibu kutegemea mahitaji ya hoja inayojadiliwa. Kwa msingi huu si antonimu zote zilizokusanywa zimetumika moja kwa moja kushadidia hoja. Data za makala haya zimechanganuliwa kwa mikabala ya kitaamuli na kitakwimu. Katika mkabala wa kitakwimu mtafiti ametumia mbinu za uchanganuzi tija na upangiliaji. Hapa mtafiti alichunguza data zote na kuziteua zile zenye tija katika hoja za makala hii. Vilevile, data zilipangiliwa kidarajia kulingana na sifa zake. Upangiliaji huo ulisaidia kuzipata data zenye sifa zinazohitajika wakati wa uelezaji wa hoja. Mbinu ya maelezo imetumika katika mkabala wa kitakwimu wakati wa kudokeza kiasi gani kanuni fulani zimevunjwa kwenye kueleza kwa vinyume maana za vidahizo vya KKK3.

**Mkabala wa Kinadharia**

Uchanganuzi wa data za makala hii uliongozwa na Nadharia Jumuishi ya Leksikografia (NJL) iliyoasisiwa na Herbert Wiegand mwaka 1970. NJL imejikita kueleza kuelezea kanuni za jumla zinazohusu utungaji, upitiaji na uhakiki wa kamusi mbalimbali (Wiegand, 1983). NJL imeundwa katika misingi mitatu. Mosi, ni matumizi ya maarifa ya nadharia nyingine zisizo za kileksikografia kukamilisha kazi za kamusi. Pili, ni kuzingatia mahitaji ya mlengwa wa kamusi katika kutunga, kuhakiki na kuchambua data zinazoihusu kamusi hiyo. Tatu, ni kuzingatia kuwapo kwa uhusiano wa kichambuzi katika kamusi na kanuni asilia zinazokubalika na wanaleksikografia wengine tangulizi. Yaani mtungaji na mhakiki wa kamusi hawapaswi kufanya kazi ya kamusi pasipo kuhusisha kabisa ujuzi wa kileksikografia. Katika makala haya imetumika misingi yote mitatu ili kuepusha uwezekano wa kujitokeza uchambuzi ulioegemea upande mmoja tu (wa mtungaji au mhakiki).

Hoja za makala haya zimeelezwa kwa kuzingatia matumizi ya maarifa ya nadharia nyingine zisizo za kileksikografia zinavyotumika kuingiza antonimu. Mwingiliano wa maarifa hayo na leksikografia umejikita kutimiza mahitaji ya mlengwa wa KKK3 kuzing'amua maana za vidahizo mbalimbali vilivyoingizwa katika kamusi hii. Suala la kuzingatia mawazo ya wanaleksikografia wengine limehusika pia ili kuufanya uchambuzi ujikite zaidi kwenye kanuni badala ya maoni binafsi ya mtafiti.

**Changamoto za Uingizaji wa Antonimu katika KKK3**

Katika utungaji wa kamusi hujitokeza changamoto zinazohusu vipengele mbalimbali vinavyounda vitomeo. Miongoni mwa vipengele vyenye changamoto ni matumizi ya antonimu zinazofasili vidahizo. Changamoto hizo zimegawanyika katika masuala yanayohusu idadi, mpangilio na muundo wa antonimu, ulinganifu wa kikategoria, matumizi ya alama za uakifishi, urejeleano wa kimaana na vidahizo vyote vyenye asili ya unyume kupewa antonimu.

**Kukosekana kwa Urari wa Antonimu Kiidadi**

Uingizaji wa antonimu katika KKK3 umejitokeza kwa namna tofauti kiidadi ambapo baadhi ya vidahizo vimefasiliwa kwa antonimu moja vingine zaidi ya moja. Maelezo yanayopaswa kumuongoza mlengwa wa kamusi hii yanaonesha kuwa watungaji wake walipanga kuwapo kwa idadi ya antonimu moja kwa kidahizo kimoja chenye sifa ya kufasiliwa kwa unyume. Hata hivyo, imebainika KKK3 imetumia antonimu zaidi ya moja kwenye baadhi ya fasili za vidahizo. Ukosefu wa urari wa kiidadi husababisha mwonekano wa kamusi usiofaa badala yake kamusi husika hupaswa iwe na idadi ya wastani iliyokubalika na watungaji ama wanajopo katika uelezaji wa vidahizo vyake. Tuchunguze data Na. 1-5.

1. **chelewa**[1] **chelew.a** */ʧɛ`lɛwa/ kit.ele.* **a.** kuwa nyuma ya muda maalum uliopangwa **b**. wasili sehemu baada ya muda kupita ***meth:*** ~ ~ *utakuta mwana si wako* = anayekuwa wa kwanza hupata mambo mazuri ***kis.:*** ahirika ***kiny.:*** <u>wahi</u> ⇌ *cheleweka, chelewesha* (**Chanzo**: BAKITA, 2022: 120).
2. **baraka**[1] */ba`ra:ka/ nm.* (*Ø*) {*i-/zi-*} jumla ya mambo yote mazuri katika maisha ya mtu ***vis.:*** neema, fanaka ***viny.:*** <u>mikosi</u>, <u>nuksi</u> (**Chanzo**: BAKITA, 2022: 62).
3. **rahisi**[2] */ra`hisi/ kiv.* **a.** enye gharama nafuu, -siokuwa <u>ghali</u> **b.** – siokuwa na <u>ugumu</u>, - isiyo <u>imara</u>; nyonge, - epesi ***meth.:*** ~ *haihalisi*
(**Chanzo**: BAKITA, 2022: 854).
4. **hafidhina** */hafi`ðina/ nm.* (*wa-*) {*a-/wa-*} pia **mhafidhina** mtu mwenye kushikilia mambo ya kale; mtu asiyependa mabadiliko ***viny.:*** <u>mwanausasa</u>, <u>mmamboleo</u>, <u>mwanamageuzi</u>, <u>mpenda mabadiliko</u> ► Kiar
(**Chanzo**: BAKITA, 2022: 266).

5. **pinga ping.a** */ˋpiŋga/ kit.ele.* pia **pinza a.** kata hoja, uamuzi, Mawazo au utekelezaji wa jambo fulani unaofanywa na mtu, taasisi, shirika, chama au serikali ***vis.:*** kaidi, zuia, bishana, kanusha, kana, kinga, kinza ***viny.:*** <u>kubali</u>, <u>kiri</u>, <u>afiki</u>, <u>ruhusu</u>, <u>ridhia</u> **b.** wekeana mali na mtu kimakubaliano kuwa atakayetabiri kwa usahihi k.v. matokeo ya michezo achukue mali hizo ⇌ *pingia, pingiwa, pingisha* (**Chanzo**: BAKITA, 2022: 835).

Data Na. 2-5 inawakilisha vidahizo ambavyo ufafanuzi wake haujazingatia idadi ya kidahizo kimoja kwa antonimu moja. Data Na. 2 ina antonimu mbili. Data Na. 3 ina antonimu tatu. Data Na. 4 ina antonimu nne na data Na. 5 ina antonimu tano. Kwa ujumla imebainika vidahizo 118 (sawa na 31.13% ya 379) vimeingiza antonimu zaidi ya moja ilhali mwongozo wa mtumiaji wa KKK3 inaonesha kuwa uingizaji ulipaswa uwe na antonimu mojamoja. Vidahizo hivyo vimegawanyika katika makundi ya uwili kwa vidahizo 92, utatu kwa vidahizo 13, unne kwa vidahizo 4 na utano kwa vidahizo 4. Ujitokezaji wa ruwaza zote tano za kiidadi tofauti na mwongozo huweza kumchanganya mlengwa wa KKK3 hasa ukizingatia havitajwi vigezo vya kuzipunguza ama kuziongeza antonimu kwenye ufafanuzi wa kidahizo. Kuwapo kwa ruwaza tofautitofauti za idadi ya antonimu kunakiuka kanuni asilia ya kileksikografia inayopendekeza vidahizo vifasiliwe kwa kuzingatia vigezo vilivyoteuliwa na wanajopo husika au kuvitumia vigezo majumui vya utungaji wa kamusi (hususan kamusi wahidiya).

**Upangiliaji Tofautitofauti wa Antonimu katika Kitomeo**

Katika mazingira ya kidahizo kuwa na fahiwa zaidi ya moja, watungaji wa kamusi hupaswa kuwa mahususi kuzipangilia fahiwa hizo ili kutomchanganya mtumiaji wake (Salimovic, 2021). Upangiliaji huo huzingatia vigezo kama vile mdafao wa kimatumizi, mpangilio ama muundo wa herufi zake, historia (umri) na kiwango cha urejeleano kati ya kidahizo na fahiwa husika (Jones, 2002). Katika BAKITA (2022: xxviii) imeelezwa kuwa umetumika utaratibu wa kuingiza fahiwa za kidahizo kwa mujibu wa kanuni za jumla za kileksikografia zinazosisitiza kuingiza kwanza fahiwa yenye mashiko zaidi ya nyingine kwa wakati uliopo. Katika utekelezaji wa kanuni hii, baadhi ya vitomeo vimebeba antonimu ambazo mashiko katika jamii hulingana kiuzito kiasi cha mtungaji na mtumiaji wa KKK3 kupata ugumu wakati wa kuamua antonimu ipi hufaa zaidi kwa wakati uliopo. Tuchunguze data Na. 6 yenye kidahizo '**pinga**' na antonimu zake '*kubali*', '*kiri*', '*afiki*', '*ruhusu*' na '*ridhia*'.

6. **pinga ping.a** */ˋpiŋga/ kit.ele.* pia **pinza a.** kata hoja, uamuzi, mawazo au utekelezaji wa jambo fulani unaofanywa na mtu, taasisi, shirika, chama au serikali ***vis.:*** kaidi, zuia, bishana, kanusha, kana, kinga, kinza ***viny.:*** <u>kubali</u>, <u>kiri</u>, <u>afiki</u>, <u>ruhusu</u>, <u>ridhia</u> **b.** wekeana mali na mtu kimakubaliano kuwa atakayetabiri kwa usahihi k.v. matokeo ya michezo achukue mali hizo ⇌ *pingia, pingiwa, pingisha* (**Chanzo**: BAKITA, 2022: 835).

Katika data Na. 6 antonimu zilizotumika huweza kutumia kisawia katika jamii kwa wakati uliopo kiasi cha kushindwa kuamua ni neno lipi hasa limepata mashiko zaidi. Kuelekeana huko kimatumizi kunaweza kuamua antonimu ipi ianze kuingizwa na zipi zifuate kwa sababu muktadha wake kimatumizi hautofautiani. Vilevile, vipo vidahizo ambavyo antonimu zake zimeingizwa kwa kukiuka kanuni ya kiwango cha mdafao au mashiko zaidi ya kimatumizi. Katika mazingira haya neno lenye mashiko zaidi hufuata kwenye lile la matumizi machache (lisilosikika sana). Tuchunguze data Na. 7 yenye kidahizo '**abu**' na antonimu zake '*nina*' na '*mama*'.

7. **abu /***ˋa:bu/ nm.* (*Ø*) {*a-/wa-*} (*kish.*) mzazi mwanaume ***kis.:*** baba ***viny.:*** <u>nina</u>, <u>mama</u> ►Kiar (**Chanzo**: BAKITA, 2022: 3).

Kwa kurejelea data Na. 7 matumizi ya neno '*mama*' ni mapema zaidi katika jamii ukilinganisha na '*nina*' lakini lenye mdafao mdogo ndilo limetangulizwa. Kutangulizwa kwa neno lisilo na mashiko zaidi kunaweza kuathiri ujengwaji wa maana kwa mlengwa wa KKK3. Pamoja na NJL yametumika maarifa ya kiisimujamii yanayohusu viwango vya matumizi ya maneno katika jamii. Maarifa haya ya kiisimujamii yamechangia kubaini changamoto za mpangilio unaokinzana na maelekezo ya mwongozo wa mtumiaji wa KKK3.

**Mabadiliko ya Kikategoria katika Kidahizo na Antonimu**
Urari wa kikategoria kati ya kidahizo na antonimu ni miongoni mwa kanuni muhimu inayopaswa kuzingatiwa wakati wa utomeshaji wa kamusi wahidiya (Murphy, 2003). Kategoria hizo zinapobadilishwa huweza kuathiri maana inayobebwa na maneno hayo kwa kuyapunguzia uzito wake au kuondoa kabisa maana iliyopaswa kuwapo. Makala haya yameeleza kuwa vidahizo 52 kati ya 379 (sawa na 13.72%) vimebadili kategoria kwenye antonimu zilizotumika kuvifafanua. Miongoni mwa vidahizo hivyo ni ‘**shinde**’ (V) na antonimu yake ‘*mshindi*’ (N) kama inavyoonekana katika data namba 8.

8. **shinde** */ˈʃindɛ/* kiv. iliyoshindwa, mshindwa ***kiny.:*** mshindi
(**Chanzo**: BAKITA, 2022: 904).

Katika data Na. 8 mabadiliko ya kikategoria yamejitokeza ambapo kidahizo ‘**shinde**’ ni kivumishi kinachoonesha hali ya kushindwa ama kufaulu ilhali antonimu yake ‘*mshindi*’ inaonesha mtu aliyefaulu au aliyefanikiwa jambo. Pamoja na kwamba maneno haya yameonesha dhana ya kufanikiwa na kutofanikiwa vijenzi vyake kimofolojia vimesababisha mabadiliko ya kikategoria kutoka kivumishi kwenda nomino. Kwa mujibu wa NJL maana ya msingi inayobebwa kwenye mabadiliko ya maneno hayo huweza kutoeleweka kwa mlengwa wa KKK3. Hivyo, watungaji wa kamusi ni muhimu kuzingatia matumizi ya kategoria ambazo hazitamsababishia ukakasi mlengwa wa kamusi husika.

**Kutozingatia Matumizi Sahihi ya Alama za Uakifishi**
Alama za uakifishi ni muhimu katika ujenzi wa kamusi yoyote ile hususan wakati wa utomeshaji ili kurahisisha kueleweka kwa maana za vidahizo kama inavyotegemewa na mlengwa wa kamusi husika. Alama hizi ni kama vile nukta (za aina zote), herufi (kubwa na ndogo), namba juu ama namba kipeo, namba chini, vidokezi vya miiko na alama ya wimbi. Katika muktadha wa makala haya alama inayorejelewa kukiukwa ni matumizi ya namba kipeo inayotumika kupambanua zaidi kidahizo kinachorejelewa. Ukosefu wa namba kipeo umesababisha maana inayorejelewa kutokuwa bayana zaidi kwa mlengwa wa KKK3. Kidahizo kinachorejelewa kisipopambanuliwa waziwazi hukiuka msingi wa NJL unaomtaka mtungaji wa kamusi azingatie kikamilifu mahitaji ya mlengwa hususan kupatikana kwa neno na maana yake. Baadhi ya vidahizo vyenye changamoto ya kutotumia namba vipeo inahusu jozi za ‘**auni$^{1}$**’ na ‘**dhuru**’, **baathi$^{1}$**’ na ‘**fisha**’, ‘**bin$^{2}$**’ na ‘**binti**’, ‘**chache$^{2\text{ na }3}$**’ na ‘**-ingi**’, ‘**dada**’ na ‘**kaka$^{1}$**’, ‘**fila$^{1}$**’ na ‘**lila**’. Tuchunguze data namba 9 na 10 inayotokana na vidahizo **‘auni$^{1}$**’ na ‘**dhuru**’.

9. **auni$^{1}$ aun.i** */aˈuni/ kit. ele.* hudumia, okoa kitu au kiumbe kutoka kwenye janga; saidia ***mat.:*** Rajabu ameni ~ kwenye moto. ***kis.:*** nusuru ***kiny.:*** dhuru ⇌ *aunia*, *aunika*, *auniana*, *aunisha*, *aunishiwa*
(**Chanzo**: BAKITA, 2022: 42).

10. **dhuru dhur.u** */ˈðuru/ kit. ele.* **a.** fanya uharibifu kwa mtu au mnyama; athiri vibaya afya au hali ya kiumbe ***kis.:*** hasiri ***kiny.:*** auni **b.** sababisha kutokea kwa athari mbaya ⇌ *dhuria*, *dhurika*, *dhuriwa*, *dhuriana*, *dhurisha*
►Kiar (**Chanzo**: BAKITA, 2022: 163).

Data Na. 9 na 10 zinaonesha uduara uliopo kwenye vidahizo ‘**auni$^{1}$**’ na ‘**dhuru**’. Baada ya antonimu kuingizwa kwenye kidahizo kilichotangulia kialfabeti antonimu hiyo yaani ‘*dhuru*’ imeunda kitomeo huku ikiwa na antonimu ‘*auni*’ ambayo hapo awali ilikuwa kidahizo. Pamoja na kwamba imeingizwa kusaidia uimarishaji wa maana, imebainika kidahizo ‘**dhuru**’ hakijaingiza namba kipeo inayoibainisha fahiwa inayoiwakilisha homonimu **auni$^{1}$**. Namba hizo zinapokosekana huweza kumchanganya mlengwa wa KKK3 kuipata moja kwa moja maana inayolengwa hasa. Kuwapo kwa dosari za kiuakifishi katika andiko lolote rasmi kunakwamisha ujumbe kumfikia kiusahihi mlengwa (Stephano, 2017). Changamoto hii inaweza kuondolewa kwa kuongeza umakini wakati wa kuhariri na kutomesha kamusi ili ziwepo alama zote zinazopaswa kukijenga kitomeo. Wahariri na watomeshaji

wanatakiwa kupata muda wa kuitosha ratiba yao kulingana na nguvukazi ili kuongeza umakini wakati wa kuipitia kamusi husika.

**Kuwapo kwa Upendeleo wa Kileksikografia**

Katika utungaji wa kamusi, vidahizo vyote hupaswa kuwa na hadhi sawa kiasi cha kuzifanya taarifa zilizoingizwa kwenye vitomeo husika zisitofautiane kimwonekano, kiutokezaji na kiviwango. Hata hivyo, hutokea upendeleo wa kileksikografia ambapo kitomeo kimoja hujazwa zaidi taarifa kuliko vingine tofauti na misingi ama vigezo vilivyowekwa na wanajopo. Miongoni mwa upendeleo huo ni baadhi ya vidahizo kupewa antonimu ilhali vingine havipewi taarifa hizo licha ya kuwa na sifa za unyume. Katika KKK3 imebainika kuwapo kwa changamoto ya kutobainishwa kwa vigezo vya msingi vilivyotumika kuziunda na kuzipata antonimu. Wataalamu kama vile Zgusta (1992), Atkins & Rundell (2008) wanapendekeza kukitosheleza kidahizo kwa kuingiza taarifa zake zote zinazosaidia kuunda ukamilifu wa maana husika. Upendeleo wa kileksikografia umesababisha vidahizo kama vile '**chaudere**', '**ficha**' na 'y**aya**' vikose kabisa antonimu ambazo kiasili zingeweza kuboresha zaidi maana ama ufafanuzi wake. Tuchunguze data namba 11 kwa ufafanuzi zaidi.

11. **chaudere** /ʧau`dɛrɛ/ *nm.* (*ma-*) {*a-/wa-*} pia **chudere** mtoto wa kwanza kuzaliwa; kifungua mimba ***mat.:*** *~ wangu sasa anasoma kidato cha kwanza* (**Chanzo**: BAKITA, 2022: 115).

Kidahizo cha data Na. 11 kina asili ya unyume kiasi cha kuhitaji antonimu kuimarisha ufafanuzi wake ili kieleweke zaidi kwa mlengwa wa KKK3. Kutoingiza taarifa yake ya kiantonimu ilhali ipo (yaani, kitindamimba) kunaweza kuathiri kutopatikana haraka kwa maana yake. Vilevile, vipo vidahizo vilivyopunguzwa zaidi idadi ya antonimu zake ilhali vingine vimeachwa na antonimu zote zinazokihusu. Kwa kuwa mwongozo wa KKK3 haujadokeza msingi wa kuamua idadi ya antonimu kwa kila kidahizo, ni dhahiri kwamba vipo vitomeo vilivyopendelewa zaidi katika ujazo wa taarifa zake. Ili kuondoa upendeleo huo, NJL inadokeza watomeshaji ni muhimu wawe na vigezo mahususi vitakavyofuatwa kwenye vidahizo vyote kiasi cha kuifanya kamusi inayotungwa imvutie mlengwa wake kwa msingi wa urari wa taarifa za kikamusi (zikiwa ni pamoja na antonimu).

**Mpishano wa Kidhana kati ya Kidahizo na Antonimu**

Ufafanuzi wa jumla wa vidahizo hutakiwa uwe na urari na mshikamano wa kidhana kati ya kifasiliwa (kidahizo) na kifasili (antonimu) ili kutomtatiza mlengwa wa kamusi inayotungwa. Licha ya kuwapo angalizo hilo, imebainika baadhi ya vitomeo vya KKK3 vinajumuisha darajia zote za unyume hali inayosababisha kupishana kidhana kati ya kidahizo na antonimu yake. Mjumuisho wa kidhana usioendana kati ya kidahizo na antonimu huweza kumtatiza mlengwa wa kamusi kung'amua moja kwa moja maana iliyokusudiwa. Kutatiza maana aghalabu kumejitokeza kwenye antonimu zisizokuwa na mipaka maalumu inayokifasili kidahizo husika. Tuchunguze data namba 12 na 13 zinazohusu kidahizo '**uzee**' na antonimu yake '*ujana*'.

12. **uzee** */u`zɛɛ/ nm.* (*Ø*) {*u-*} **a.** hali ya kuwa na umri mkubwa kwa kuishi miaka mingi ***mat.:*** *Alijiandaa vizuri hivyo hakupata taabu katika ~ wake.* ***vis.:*** ushaibu, ukongwe, uhenga ***kiny.:*** <u>ujana</u> **b.** hali ya kutumika kwa muda mrefu ***mat.:*** *Kanga yake bado inang'aa pamoja na ~ wake* (**Chanzo:** BAKITA, 2022: 1114).

13. **ujana** */u`ɟa:na/ nm.* (*Ø*) {*u-*} **a.** kipindi cha maisha ya mwanadamu kilicho kati ya utoto na utu uzima **b.** hali ya kuwa kijana ***meth.:*** *~ ni moshi ukienda haurudi* = maisha ya ujana ni muda kitambo kidogo tu, yanapita upesi **ch.** tabia ya mtu kupenda mambo ya anasa na starehe ► Kiar **(Chanzo:** BAKITA, 2022: 1042).

Data Na. 12 inaonesha fasili ya kidahizo '**uzee**' kilivyokosa mipaka halisi ya kiufafanuzi kwa sababu katika sayansi ya kawaida mtu hupitia hatua mbalimbali za ukuaji kuanzia utoto, ujana, utu uzima kisha uzee. Kwa kuwa ngazi ya awali 'utoto' haijadokezwa kama antonimu ya kidahizo husika,

mlengwa wa KKK3 atashindwa kuing'amua moja kwa moja maana iliyoshikana na ile ya ujana kama ilivyooneshwa katika data Na. 13.

Vilevile, imebainika kuwa katika baadhi ya vitomeo vya KKK3 uhusiano huo haujaoneshwa ipasavyo. Hali hii imesababishwa na dhana zilizobebwa katika antonimu kutofumbata moja kwa moja maana iliyopo katika kidahizo. Kimsingi zipo jozi ambazo maana zake hazishikani badala yake zinakinzana ama zipo tofauti hivyo huweza kumtatiza mtumiaji wa kamusi hii kwa kudondosha baadhi ya dhana muhimu. Tuchunguze mifano ya vidahizo '**sasa**[1]' na '**baadaye**' kama inavyoonekana katika data namba 14 na 15.

14. **sasa**[1] */`sa:sa/ kiel.* wakati uliopo; muda huu **mat.:** *Ndege imewasili* ~. ***kiny***.: baadaye ► Kiar
**(Chanzo:** BAKITA, 2022: 885)

15. **baadaye** */baa`da:jɛ/ kiel.* wakati au muda wowote ujao kuanzia sasa **mat.:** *tutaonana* ~. ***kis*.:** halafu ►Kiar
**(Chanzo:** BAKITA, 2022: 44)

Katika data Na. 14 na 15 antonimu '**baadaye**' haioneshi pande zote ambazo ni vinyume vya kidahizo '**sasa**[1]' kwa kuwa imejikita tu kwenye '*wakati ujao*' ilhali inaweza kutokea hata kwa '*wakati uliopita*' au '*kabla ya*'. Hali hii inatokana na kidahizo hicho kusimama kama ndicho kipimo cha wakati ndani ya kitomeo hicho. Mtafiti anafahamu kuwapo uwezekano wa kukosa neno sahihi ambalo lingefaa kama antonimu ya pili ya kidahizo '**sasa**[1]'. Kwa hiyo, watungaji wa kamusi walipaswa kutumia maarifa ya teminografia ili kupata neno husika na kuepuka kuegemea kwenye kinyume cha '*wakati ujao*' tu.

**Kubadilika kwa Muonekano wa Umbo la Kidahizo na Antonimu**

Katika utungaji wa kamusi wahidiya ni muhimu kuwa na ulinganifu wa kiumbo kati ya kidahizo na antonimu. Makala haya yamebaini kuwa, KKK3 imeikiuka kanuni ya ulinganifu wa kiumbo katika vidahizo 111 (sawa na 29.29%) ya 379. Utofauti wa umbo (saizi) ya kidahizo na antonimu zake umejitokeza zaidi katika vitomeo vyenye asili ya vivumishi. Hali hii imesababishwa na asili ya leksimu hizo kuhitaji fasili iliyoambatana na vikanushi au kifungu cha maneno kilichoibeba dhana iliyokanushwa. Licha ya kuegemea zaidi kwenye vivumishi, zipo pia leksimu za kategoria nyingine zilizokiuka kanuni ya ulinganifu wa kiumbo. Kwa mfano kidahizo '**hafidhina**' na antonimu zake '*mwanausasa*', '*mmamboleo*', '*mwanamageuzi*' na '*mpenda mabadiliko*' ni miongoni mwa vilivyokiuka kanuni hii. Data namba 16 inathibitisha ukiukwaji huo.

16. **hafidhina** */hafi`ðina/ nm.* (*wa*-) {*a-/wa-*} pia **mhafidhina** mtu mwenye kushikilia mambo ya kale; mtu asiyependa mabadiliko ***viny.:*** mwanausasa, mmamboleo, mwanamageuzi, mpenda mabadiliko ►Kiar (**Chanzo**: BAKITA, 2022: 266).

Data Na. 16 inaonesha mpishano wa kiumbo kati ya kidahizo na antonimu zake. Kidahizo ni leksimu sahili ilhali antonimu zake ni leksimu mwambatano kwani zimepatikana baada ya kuunganisha maneno mawili ili kupata dhana ya unyume. Licha ya lengo zuri la kutaka kidahizo husika kieleweke zaidi, wanajopo walipaswa kutumia leksimu sahili zilizo sawa kimuonekano na kidahizo. Endapo asili ya lugha ndiyo iliwalazimisha, basi antonimu moja tu mwambatano yenye mashiko zaidi kimatumizi ndiyo ilipaswa kuingizwa katika kitomeo hiki. Kukiuka kanuni ya kiumbo baina ya leksimu kumetahadharishwa na wanaisimu kama vile Jones & Murphy (2005). Maoni ya wanaisimu hawa ni muhimu yazingatiwe ili kupata kamusi inayovutia, yenye vitomeo vya kutosha na vinavyoeleweka kwa mlengwa wa kamusi husika kulingana na misingi ya NJL.

**Hitimisho**

Kwa ujumla, imedhihirika kwamba matumizi ya antonimu katika kamusi wahidiya (za Kiswahili) huambatana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwake ni zile zinazohusu idadi ya antonimu, mabadiliko ya kategoria, mpangilio wa antonimu, mpishano wa kidhana, upendeleo wa kileksikografia na matumizi yasiyo sahihi ya alama za uakifishi. Changamoto hizo zimesababisha kukosekana kwa urari wa matumizi sahihi ya kanuni za kuingiza antonimu katika KKK3 kiasi cha kuweza kuathiri baadhi ya fasili na muonekano wa jumla wa vitomeo vya unyume. Kukithiri kwa changamoto za kikanuni ndani ya kamusi huathiri uzito wa maana za vidahizo zilizokusudiwa kumfikia mlengwa wa kamusi husika. Kwa msingi huo, kuna kila haja kwa watungaji wa kamusi kuongeza umakini na kuzingatia kanuni zote walizojiwekea lakini zinazokubalika na wanaleksikografia tangulizi wakati wa utomeshaji wa vinyume hususan kwenye kamusi wahidiya.

**Marejeleo**

Atkins, B. T. & Rundell, M. (2008). *The Oxford guide to practical lexicography*. New York: Oxford University Press.

BAKITA, (2022). *Kamusi Kuu ya Kiswahili (Toleo la 3)*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers PLC.

Bezuglova, O. A. (2020). On compiling a dictionary of phraseological antonyms. *Modern Journal of Language Teaching Methods Special Issues ELT in Russia,* 151 - 154.

Bowern, C. (2008). *Linguistic fieldwork: A practical guide*. London: Palgrave Mcmilan.

Fellbaum, C. (1995). Co-occurrence and antonymy. *Journal of Lexicography*, 8 (4), 281- 303.

Fellbaum, C. (2016). The treatment of multiword units in lexicography. Katika P. Durkin (Mh.) *The Oxford Handbook of Lexicography* (kur. 411 - 424). Oxford: OUP.

Jackson, H. (2002). *Lexicography: An Introduction*. London: Taylor and Francis Routledge.

Jones, S. (1986). *Synonymy and semantic classification*. Edinburg: Edinburg University Press

Jones, S. (2002). *Antonym: A corpus-based perspective.* Amsterdam: Routledge.

Jones, S. & Murphy, L. M. (2005). Using corpora to investigate antonymy acquisition. *International Journal of Corpus Linguistic*, 10 (3), 401 – 422.

Keifer, F. & Sterkenburg, P. (2003). Design and production of monolingual dictionaries.

Katika P. Sterkenburg (Mh.) *A Practical Guide to Lexicography* (kur. 350-365). Amsterdam: JB Publishing Company.

Lehrer, S. (1974). *Semantic fields and lexical structures*. Amsterdam: Holland Print.

Lobanova, A., Tom, K. & Jennifer, S. (2010). Defining antonymy: A corpus-based study of opposites by lexico-syntactic patterns. *International Journal of Lexicography,* 23 (1), 19 - 53.

Murphy, L. M. (2003). *Semantic relations and the lexicon: Antonyms, synonyms and other semantic paradigms*. Cambridge: Cambridge University Press.

Okal, B. (2019). Matumizi ya vielelezo vya kihisabati katika fafanuzi za fahiwa mbalimbali. *Jarida la Mwanga wa Lugha*, 3 (1), 41 - 62.

Paradis, C. & Willners, C. (2011). Antonymy: From conventionalization to meaning making. *Review of Cognitive Linguistics*, 9 (2), 367 - 391.

Salimovic, S. S. (2021). Lexicography and dictionary compilation. *Linguistics,* 22, 52-66.

Stephano, R. (2017). *Uzingatizi wa viakifishi katika uandishi wa kitaaluma: Mifano kutoka shule za msingi Tanzania*. Tazimili ya uzamivu. Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

Sterkenburg, P. (2003). Onomasiological specifications and a concise history of onomasiological dictionaries. Katika P. Sterkenburg (Mh.) *A Practical Guide to Lexicography* (kur. 127-144). Amsterdam: JB Publishing Company.

TUKI, (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 4). Nairobi: OUP East Africa Ltd.

Wiegand, H. E. (1983). On the structure and contents of a general theory of lexicography. Katika R. K. Hartmann (Mh.) *Lexeter Proceedings* (kur. 13-30). Tubingen. Max Verlag.

Zgusta, L. (1992). *History, language and lexicographers*. Tubingen: Niemeyer.